

# SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Simu: 2133428

Nukushi: 2133990

Barua pepe:- [dq@tr.co.tz](mailto:dq@tr.co.tz)



Ofisi ya Uhusiano,

S.L.P. 70364,

Dar Es Salaam

---

## YAH: TAARIFA YA AJALI YA TRENI B17 NA KICHWA CHA TRENI CHENYE NAMBA 9004

**Dar Es Salaam Tarehe 3 Januari 2021**

Uongozi wa Shirika la Reli Tanzania (TRC) Unasikitika Kutangaza tukio la Ajali lilitokea Maeneo ya Kigwe-Bahi umbali wa Kilomita 508 Kutokea Dar Es Alaam na Kilomita 58 Kutokea Dodoma, Treni hiyo ilikuwa inatokea jijini Dar Es Salaam ikielekea Mikoa ya Tabora, Katavi (Mpanda), Kigoma na Mwanza ikiwa na Abiria wapatao 720.

Treni hii iliwasili Dodoma majira ya saa 9:15 alasiri na Kuondoka Dodoma majira ya Saa 11:40 Jioni. Treni hii iliwasili katika kituo cha Kigwe majira ya saa 12:25 Jioni na Kuondoka saa 12:27 Jioni.

Treni hii ilikuwa na Behewa 12 na kati yake Behewa 6 ndizo zilipata ajali Usajili wake ni kama ifuatavyo:

- TCB 3603 ya kwanza kutoka kwenye kichwa cha Treni
- TCB 3612 ya Pili kutoka kwenye kichwa cha Treni
- TCB 3652 ya tatu kutoka kwenye kichwa cha Treni
- TCB 3650 ya Nne kutoka kwenye Kichwa cha Treni
- TCB 3619 ya Tano kutoka kwenye Kichwa cha Treni
- Na ya Mwisho ni yenyе Usajili wa Na. RCB 4526.

Mpaka sasa Majeruhi ni 66 na waliopoteza maisha ni watatu (3), akiwemo mtoto mmoja (1) na watu wazima wawili (2).

Majeruhi wamekwisha chukuliwa eneo la Tukio na wanaendelea na matibabu katika Hospitali za Bahi na hospitali ya Mikoa wa Dodoma.

Uchunguzi wa Chanzo cha ajali unaendelea kufanyika na Shirika litaendelea kutoa Taarifa.

Uongozi wa Shirika la Reli unatoa Pole kwa Abiria wote waliofikwa na ajali, Majeruhi na Ndugu na Jamaa waliopoteza Wapendwa wao.

A handwritten signature in black ink, enclosed in a small oval border.

Jamila Mbarouk  
Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano